KATC TAARIFA

Umwagiliaji Maji Mashambani kwa Maendeleo ya Kilimo

KILIMANJARO AGRICULTURAL TRAINING CENTRE (KATC) - MOSHI
S.L.P. 1241 Moshi—Simu 255-27-2752293
Baruapepe: katc@kilionline.com

Toleo Na. 1 | Julai/Agosti 2003

Chuo cha Kilimo cha Kilimanjaro (KATC) - Moshi

Mkuu wa Chuo Nd. R.J. Shayo, akisisitiza jambo wakati wa Ufunguzi wa Kozi ya Wakulima Viongozi

Kilimanjaro Agricultural Training Centre (KATC)−Moshi ni moja ya vyuo saba vya Wizara ya Kilimo na Chakula, ambacho kinajishughulisha na kuendesha kozi fupi za kilimo cha umwagiliaji maji mashambani hususan kwa zao la mpunga.

Chuo hiki kiko katika kijiji cha Chekereni, kata ya Mabogini, wilaya ya Moshi Vijijini, Mkoa wa Kilimanjaro, umbali wa kilometa 18 kusini mashariki ya mji wa Moshi. Chuo kina madarasa, maabara, maktaba, ofisi na mabweni yenye uwezo wa kulaza washiriki sitini wa kozi mbalimbali kwa wakati mmoja. Kozi zinazoendeshwa na chuo cha KATC ni pamoja na; *kilimo bora cha mpunga kwa njia ya umwagiliaji, matumizi bora ya maji mashambani, matumizi bora ya zana za kilimo na uendeshaji mzuri wa skimu za umwagiliaji*. Kozi hizi ni maalum kwa ajili ya wakulima wamwagiliaji, maafisa ugani wanaofanya kazi katika skimu za umwagiliaji, maafisa umwagiliaji, wataalam wa zana za kilimo, viongozi wa vyama vya wakulima wamwagiliaji na mameneja wa skimu za umwagiliaji. Muda wa mafunzo ni majuma mawili hadi manne kulingana na aina ya kozi.

Chuo cha KATC kilianzishwa tarehe 1 Julai 1994, baada ya uongozi wa Mkoa wa Kilimanjaro kukabidhi kwa Wizara ya Kilimo baadhi ya majengo na vifaa vilivyokuwa vikitumiwa na Mradi wa Umwagiliaji wa Lower Moshi ili vitumike kusambaza teknolojia ya kilimo bora cha mpunga kwa njia ya umwagiliaji nchi nzima kwa njia ya mafunzo. Baada ya kukabidhiwa chuo hiki na kukifanya kuwa cha kitaifa, Serikali ya Tanzania kupitia Wizara ya Kilimo iliendelea kushirikiana na Serikali ya Japan

Jengo la Utawala la Chuo cha KATC Chekereni

kupitia Shirika lake la Misaada ya Kimataifa la JICA kukiendesha kama Mradi wa KATC.

Kazi hii ilifanyika kwa mafanikio mazuri chini ya Mradi wa KATC Awamu ya Kwanza uliomalizika June 2001. Baada ya hapo, Mradi wa KATC Awamu ya Pili ulianzishwa mwezi October 2001 na unatarajiwa kumalizika September 2006.Madhumuni ya Mradi wa KATC Awamu ya Pili ni kuziendeleza skimu sita, (moja kutoka kila kanda ya umwagiliaji Tanzania Bara) kuwa za mfano kwa skimu nyingine zote nchini kwa kuzipa utaalam katika uzalishaji, matumizi bora ya maji mashambani na uendeshaji mzuri wa umoja wa wamwagiliaji na skimu kwa ujumla.
Mbinu iliyobuniwa ya kuyafikia malengo ya Mradi ni;

- Kutembelea skimu zote sita na kuibua matatizo yanayokwamisha uzalishaji kwa kutumia mbinu shirikishi jamii.
- Kuendesha mafunzo kwa wakulima viongozi 20 kutoka kila skimu wakiwa pamoja na wataalam wao, ili kuwawezesha kuhamasisha uundaji wa vikundi vidogovidogo na wao kuwa wawezeshaji ndani ya vikundi hivyo.
- Kufuatilia uundaji wa vikundi vya wakulima wa mfano, kutoa ushauri kwa wakulima viongozi na kushiriki kuendesha mafunzo kwa wakulima wa mfano.
- Kuhamasisha wakulima wa mfano kuendelea kusambaza utaalam kwa wakulima wengine bila uchoyo (farmer to farmer extension), kwa matarajio kwamba baada ya muda si mrefu skimu nzima itakuwa inalima kitaalam.
- Kuanzisha mashamba ya majaribio ili

Yaliyomo katika toleo hili:

- **Sera ya Uchangiaji Gharama**
- **Uenezaji Ushauri kwa Wakulima**
- **Wakulima viongozi**
- **Jinsia katika mafunzo**

kuhakikisha kwamba utaalam utakaohimizwa ni ule tu unaoendana na hali halisi na mazingira ya skimu husika.

- Kuwahamasisha wakulima viongozi kuanzisha mashamba ya mfano ili kuwawezesha kuendesha mafunzo kwa vitendo.
- Kuwahusisha kikamilifu wadau wote wa skimu za mfano, zikiwemo halmashauri za wilaya husika na wahandisi wa umwagiliaji – kanda ili wahamasike kutumia mbinu za Mradi wa KATC Awamu ya Pili kusambaza utaalam kutoka katika skimu za mfano kwenda katika skimu nyingine.
- Ili mbinu za Mradi wa KATC Awamu ya Pili ziwe endelevu, Mradi unasisitiza umuhimu wa wadau wote kuchangia gharama.

Mradi wa KATC Awamu ya Pili unajihusisha pia na maendeleo ya kilimo cha umwagiliaji katika nchi jirani za Kenya, Malawi, Uganda na Zambia. Mbinu zinazotumika ni zile zile ila kila nchi jirani imepangiwa kuanza na skimu moja tu ya mfano. Ifuatayo ni orodha ya skimu teule zinazoshiriki Mradi wa KATC Awamu ya Pili pamoja na nchi au kanda ya umwagiliaji husika katika mabano:
Skimu ya umwagiliaji Mombo - Korogwe (Kanda ya Kilimanjaro), Skimu ya umwagiliaji Mwega – Kilosa (Kanda ya Morogoro), Skimu ya umwagiliaji Mbuyuni – Mbarali (Kanda ya Mbeya), Skimu ya umwagiliaji Nakahuga – Songea (Kanda ya Mtwara), Skimu ya umwagiliaji Mwamapuli – Igunga (Kanda ya Tabora), Skimu ya umwagiliaji Nduguti – Shinyanga Vijijini (Kanda ya Mwanza), Skimu ya umwagiliaji ya South West Kano – (Kenya), Skimu ya umwagiliaji ya Doho – (Uganda), Skimu ya umwagiliaji ya Bwanje Valley – (Malawi) na Skimu ya umwagiliaji ya Sefula – (Zambia).

Lengo kuu la Mradi wa KATC Awamu ya Pili ni kuboresha maisha ya mkulima anayelima kwa njia ya umwagiliaji kwa kumpa utaalam utakaomwezesha kuzalisha kwa faida. Kwa kuzingatia ukweli kwamba miradi ya umwagiliaji ni miradi inayojengwa kwa gharama kubwa, ni busara kuhakikisha kwamba wakulima ndani ya miradi hii wanazalisha kwa kiwango cha juu kadiri iwezekanavyo. Hata hivyo, ni lazima wakulima hao wawe wameunda chombo cha kuwaunganisha, kitakachotunga na kusimamia taratibu za matumizi bora ya maji mashambani. Uongozi bora wa kidemokrasia ndani ya vyombo hivyo nao ni muhimu. Mitaala ya Chuo cha KATC inashughulika na masuala hayo yote.

Kwa Wasomaji

Kwa kutumia anwani yetu (uk. 1) tuleteeni Ushauri, Maoni au Habari ili kuboresha jarida hili.

Sera ya Uchangiaji Gharama katika Skimu za Mfano

Na Hirotoshi KODA – Mshauri Mkuu wa Mradi KATC II

Nd. H. Koda akijadiliana na Washiriki wa Kozi

Uchangiaji gharama katika Miradi ya maendeleo ni sera ya taifa ambayo inalenga kuwahusisha wadau kushiriki katika kuchangia gharama za miradi hiyo.

Lengo la uchangiaji gharama ni kuwafanya wadau wote kujenga dhana ya umiliki wa miradi hiyo na kuifanya iwe endelevu kinyume na hapo awali ambapo ilionekana kuwa;miradi yote ya maendeleo ni ya wahisani na ni wao ndio wanaowajibika na uendelezaji wa miradi hiyo. Dhana hiyo potofu ilisababisha miradi mingi kufa, mara baada ya wahisani kuondoka.

Kwa kuzingatia sera hiyo, Mradi wa KATC awamu ya pili umeamua kutoa uzito wa aina yake katika kuhakikisha kuwa wadau wote wanashiriki kikamilifu katika kuchangia gharama ili kuufanya uwe endelevu.

Hivyo basi, katika warsha ya wadau wote wa mradi iliyofanyika KATC Moshi mwezi Februari 2003; wadau waliweza kuainisha majukumu na wajibu wao katika shughuli za mradi na kutoa mapendekezo yafuatayo kuhusu uchangiaji wa gharama:

- Vifaa vyote vya mafunzo, kama vifaa vya palizi vya kusukuma kwa mkono, mbolea, saruji na kokoto. Pia vifaa vya kituo cha hali ya hewa, matrekta ya mkono viandaliwe na KATC.
- Wilaya husika itaandaa pembejeo kama vile mbolea na madawa zitakazotumika wakati wa mafunzo kwa wakulima katika skimu.
- Mashamba ya mpunga kwa ajili ya maonyesho na majaribio yataandaliwa na wakulima chini ya usimamizi wa skimu na vyama vya wakulima.

Ni matumaini ya mradi kuwa dhana hii itajengeka katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kuwawezesha wananchi kumiliki miradi hiyo na kuifanya iwe endelevu hata baada ya wahisani kuondoka.

Uenezaji wa Teknolojia kwa Wakulima

Na Hanif Nzully

Katika kueneza tekinolojia ya kilimo cha mpunga kwa njia ya umwagiliaji; mradi wa KATC Awamu ya Pili umelenga zaidi katika kutoa mafunzo kwa wakulima ambao wataitwa Wakulima Viongozi. Wakulima Viongozi watahudhuria mafunzo chuoni KATC na pia watapata nafasi ya mafunzo ndani ya skimu zao. Pamoja na mambo mengine, Wakulima Viongozi watafundishwa mbinu mbali mbali za elimu ya ushauri kwa wakulima ili kuwawezesha kusambaza elimu ya kilimo bora cha mpunga waliyoipata KATC kwa wakulima wa kati na hatimaye kwa wakulima wengine kwenye skimu zao. KATC imekusudia kuwawezesha Wakulima katika skimu:

- Kutambua hali halisi ya uenezaji wa elimu ya kilimo bora katika skimu zao
- Kuibua na kutambua matatizo yanayokwamisha maendeleo yao na jinsi ya kuyatatua
- Kuwa na upeo wa kuelewa ugumu au urahisi wa majukumu yaliyo mbele yao
- Kuwa na uwezo wa kusimamia na kutathmini shughuli zao wao wenyewe

Kwa mantiki hiyo, wakulima viongozi ambao wanachaguliwa kwa utaratibu maalum ambao unafuata vigezo vilivyokubaliwa na wadau husika wataunda vikundi vya wakulima wa kati na kuwafundisha kwa kutumia mbinu mbalimbali za ugani walizofundishwa KATC.

Njia hii ya kuwatumia wakulima kuwafundisha wakulima wengine ni nzuri kwa sababu wakulima hupenda kujifunza kutoka kwa wakulima wenzao kwa kuzingatia hali halisi kuwa wanalingana kiuwezo na wanakuwa huru zaidi kwa kuwa wanaishi kwenye eneo moja

Pamoja na kuunda vikundi vya wakulima wa kati; wakulima viongozi watakuwa na mashamba ya maonyesho ambayo yatatumika kama madarasa ya kufundishia. Mashamba hayo pia yatatumika katika siku za wakulima kuonyesha mafanikio na kueneza ujumbe kwa wakulima wengine katika skimu zao.

Mfumo wa uenezaji wa mafunzo kwa wakulima kwenye Skimu za Mfano



WV	Wakulima Viongozi
WK	Wakulima wa Kati
WW	Wakulima Wengine

Mkurugenzi wa mafunzo - Wizara ya Kilimo na Chakula Nd. R.Kapande (aliyesimama) akiwahutubia wakulima viongozi katika ziara ya mafunzo iliyofanyika katika skimu ya Lekitatu wilayani Arumeru. Mkoani Arusha.

Wajue Wakulima Viongozi na Majukumu yao

Na Hanif Nzully

Mfumo wa mafunzo ya uenezaji wa tekinolojia bora ya kilimo cha mpunga kwa njia ya umwagiliaji katika mradi wa KATC awamu ya pili, unawahusisha wakulima 20 kutoka kila skimu ya mfano ambao wanajulikana kama Wakulima viongozi. Wakulima viongozi ndio ambao wanahusika moja kwa moja na mafunzo yanayotolewa na KATC, chuoni na ndani ya skimu za mfano kwa utaratibu uliowekwa na wadau husika. Wakulima hao wanachaguliwa kwa kufuata vigezo maalum ambavyo vilikubaliwa na wadau na pia wanakuwa na wajibu na majukumu maalum ambayo wanayatekeleza ili kufanikisha dhana nzima ya kuboresha kilimo cha mpunga kwa njia ya umwagiliaji.

Baadhi ya vigezo vinavyotumika kuwachagua wakulima viongozi ni kama vifuatavyo:

- Awe anajua kusoma na kuandika
- Awe na shamba la mpunga ndani ya skimu
- Awe anashiriki kikamilifu katika kilimo cha mpunga
- Awe na uwezo wa kueneza tekinolojia kwa wakulima wengine (aweze kuelekeza)
- Awe anashirikiana vizuri na akubalike na wakulima wengine
- Uwiano wa kijinsia: Kuwepo na Uwiano wa kijinsia ulio sawa katika kuwachagua.

Ili kueneza tekinolojia sahihi ya uzalishaji wa mpunga kwa njia ya umwagiliaji; mkulima kiongozi anatakiwa achukue hatua kueneza tekinolojia hiyo kwa wakulima wa kati na wakulima wengine kwa kutekeleza wajibu na majukumu yafuatayo:

- Kuhudhuria mafunzo KATC ili kupata elimu ya nadharia na vitendo katika uzalishaji bora wa mpunga na mazao mengine kwa njia ya umwagiliaji.
- Kutumia elimu na ujuzi alioupata shambani mwake na alifanye shamba lake kuwa darasa
- Kueneza elimu na ujuzi alioupata kwa wakulima wa kati na wakulima wengine katika skimu.
- Kuwa na mahusiano mazuri kwa kushirikiana na Bwana shamba na viongozi wa skimu, na pia
- Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya shughuli zote atakazozifanya.

Kwa ujumla kazi hiyo inahitaji kwa kiasi kikubwa, moyo wa kujituma ili kufanikisha zoezi zima na kufikia lengo tulilojiwekea.

Jinsia katika Mafunzo

Na Symphorose Mahendeka (KATC)

Mradi wa KATC awamu ya pili unasisitiza uwiano sawa wa kijinsia kwa washiriki wa mafunzo y o t e

Wakulima wakishiriki mafunzo kwa vitendo

yanayofanyika ndani na nje ya KATC.

Hii inajidhihirisha wazi katika vigezo vinavyotumika kuwachagua wakulima kushiriki mafunzo. Katika mafunzo ya kwanza ya wakulima viongozi toka skimu za Mombo na Nakahuga yaliyofanyika mwezi Machi 2003, kulikuwa na uwiano sawa wa kijinsia kwa washiriki. Jumla ya wanawake 10 na wanaume 10 toka kila skimu waliweza kushiriki kwenye mafunzo hayo na kufanya kigezo hicho kifanikiwe kwa asilimia mia moja.

Kwa kuzingatia wajibu na majukumu ya wanawake katika shughuli za kilimo katika familia nyingi hapa nchini, Mradi wa KATC awamu ya pili umeamua kutilia mkazo suala la wanawake walioko kwenye skimu sita [6] za mfano zilizochaguliwa, wanashiriki bega kwa bega na wakulima wenzao wa

Ratiba ya Mafunzo - Julai 2003 hadi Oktoba 2003

Aina ya mafunzo	Tarehe	Washiriki	Skimu husika
Mafunzo KATC	28/7-15/8/2003	Wakulima viongozi	Mwega na Mbuyuni
Mafunzo katika skimu (awamu 1)	1-5/9/2003	Wakulima wa kati	Mombo
Mafunzo katika skimu (awamu 2)	29/9-3/10/2003	Wakulima wa kati	Nakahuga
Mafunzo KATC	8-19/9/2003	Wakulima Viongozi na Maafisa Kilimo	S.W.Kano-Kenya & Doho–Uganda
Ushauri wa Kitaalam	6-17/10/2003	Wakulima Viongozi	S.W.Kano-Kenya & Doho-Uganda
Mafunzo KATC	13-31/10/2003	Wakulima Viongozi	Ndunguti & Mwamapuli